

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA



TAMKO LA WIKI YA UHAMASISHAJI WA KUDHIBITI UVIDA (USUGU WA VIMELEA VYA MAGONJWA DHIDI YA DAWA) DUNIANI (WORLD ANTIMICROBIAL RESISTANCE AWARENESS WEEK - WAAW)  
TAREHE 18-24 NOVEMBA, 2024

**Ndugu Wananchi**, ikumbukwe kuwa, tarehe 18 hadi 24 Novemba ya kila mwaka tunaadhimisha wiki ya uhamasishaji na kuongeza uelewa juu ya kupambana na (Usugu wa Vimelea vya Magonjwa Dhidi ya Dawa) (UVIDA).

UVIDA ni hali inayotokea pale ambapo vimelea vya magonjwa kama bakteria, virusi, fangasi, parasite, n.k vinastahimili nguvu ya dawa iliyokusudiwa kuvua vimelea hivyo. Dawa zinazoathirika na hali hii kwa kiasi kikubwa ni dawa za antibiotiki.

**Ndugu Wananchi**, Kwa pamoja, Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Kilimo na Chakula (FAO), Shirika la Afya za wanyama (WOAH) na Shirika la Mazingira (UNEP) yametaja usugu wa vimelea dhidi ya dawa kuwa moja kati ya majanga 10 ya dunia. Zipo sababu nyingi zinazochangia kuongezeka kwa UVIDA nchini zikiwemo:

- i. Kutumia dawa kwa binadamu au mfugo bila ushauri wa mtaalamu wa afya ya binadamu na wanyama;
- ii. Kutokilishi dozi au kutotumia dawa kulingana na maelekezo ya mtaalamu ya afya;
- iii. Kutumia dawa zilizosalia kutoka matibabu ya awali kutibu ugonjwa wa sasa;
- iv. Utupaji holela wa masalia ya dawa katika mazingira;
- v. Kutozingatia usafi binafsi kama vile kuosha mikono na usafi wa mazingira kunakoweza kusababisha kuenea kwa magonjwa na hivyo matumizi ya dawa hasa antibiotiki;
- vi. Kwa wafugaji, kuuza mazao ya mifugo kama mayai, maziwa au nyama ambayo bado mifugo inatumia dawa au kipindi cha dawa (Withdrawal Period) hakijaisha kama inavyoshauriwa na mtaalamu wa mifugo; na
- vii. Kwa mtoe huduma za afya, kutoa dawa bila kufuata miongozo na bila kutoa maelekezo sahihi juu ya matumizi sahihi ya dawa.

**Ndugu Watanzania,** UVIDA usipo dhibitiwa husababisha athari nyingi kubwa za kiafya na kiuchumi ambazo ni pamoja na: ugonjwa kujirudiarudia; kutumia muda mwingi zaidi hospitalini kwa ajili ya matibabu kama kulazwa; kupunguza nguvu kazi ya uzalishaji na hivyo kupelekea kushuka kwa pato la familia na Taifa;

kuongezeka kwa gharama za matibabu kwa kutumia dawa ghari zaidi na hivyo kuathiri uchumi wetu; ulemavu wa viungo; na hata vifo kwa binadamu, mifugo na samaki.

**Ndugu wananchi**, Tafiti za kidunia pamoja na Tanzania pia zimeonesha kuwa maambukizi ya vimelea sugu yanaongeza umaskini. Hivyo, tunapaswa kuungana na Jumuiya ya Kimataifa katika maadhimisho ya wiki hii, yenyewe Kaulimbiu inayosema "**Educate, Advocate, Act now**" ikimaanisha "**Elimisha, Hamasisha, Chukua hatua sasa**". Kwa mantiki hii wote tuna jukumu la kuhamasishana kuhusu matumizi sahihi ya dawa hizo kwa ajili ya manufaa yetu ya sasa na kizazi kijacho.

**Ndugu wananchi**, UVIDA unaweza kudhibitiwa kwa njia nyingi ambazo ni rahisi kuzifuata ambazo ni:

- i. Kuzingatia ushauri wa mtaalamu wa afya badala ya kukimbilia duka la dawa kwa kila ugonjwa;
- ii. Kutumia dozi ya dawa kikamilifu kama unavyoshauriwa na mtaalamu wa afya;
- iii. Kuepuka kutumia dawa zilizosalia kutoka matibabu ya awali kutibu ugonjwa wa sasa;
- iv. Kuzingatia usafi binafsi kama kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni na usafi wa mazingira kwa ujumla ili kujikinga na magonjwa yanayopelekea kutumia dawa mara kwa mara;

- v. Kufuata maelezo ya mtaalamu wa mifugo juu ya matumizi sahihi ya dawa kwa mifugo;
- vi. Kwa wafugaji, baada ya kuwapa mifugo dawa zingatia ushauri wa mtaalamu wa mifugo kabla ya kuuza mazao yatokanayo na mifugo hao kama maziwa, mayai na nyama; na
- vii. Kuzingatia ratiba na matumizi ya chanjo kwa binadamu na mifugo ili kupunguza matumizi ya dawa **“Tukumbuke kuwa kinga ni bora kuliko tiba”**.

**Ndugu wananchi,** Serikali katika kukabiliana na changamoto hii, serikali inatekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kupambana UVIDA (National Action Plan on Antimicrobial Resistance (NAP – AMR, 2023-2028) katika dhana shirikishi ya Afya Moja.

Katika mpango kazi huu zimeainishwa afua kuu tano zenyelengo la kuongeza uelewa (AMR awareness) kama tunalolifanya leo hii hapa; ambazo ni kufanya tafiti na ufuatiliaji wa usugu (AMR research and surveillance); kukinga na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza (infection prevention and control); matumizi sahihi ya dawa (antimicrobial stewardship); pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya usugu wa vimelea dhidi ya dawa (monitoring and evaluation).

**Niwaombe wadau na watendaji wote kujikita katika kutekeleza Mpango huo ili kudhibiti UVIDA.**

**Ndugu wananchi;** Mapambano dhidi ya UVIDA yanataka ushirikiano wa dhati katika kutekeleza Mpango Kazi tulionao. Nazielekeza Taasisi na Mabaraza ya Kitaaluma kusimamia wanataaluma ili watimize majukumu yao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Miongozo na miiko ya taaluma zao; Niwaombe wanahabari tupeleka taarifa sahihi kwa umma juu ya athari za UVIDA na mbinu rahisi za kukabiliana nao; Niwaombe wananchi kuzingatia ushauri wa wataalamu kabla ya matumizi ya dawa kwao na kwa mifugo.

**Ndugu wananchi,** Niwaalike tuadhimishe maadhisho haya ya mwaka huu 2024 kwa kuhakikisha tunawafikia wananchi wengi zaidi kwenye jamii zetu kuitia asasi zisizo za kiraia na taasisi za serikali. Aidha, wanasayansi, wataalam wote katika sekta ya afya ya binadamu, mifugo, kilimo, mazingira na waandishi wa habari twendeni tukaelimisha jamii juu ya changamoto hii ili waweze kutumia dawa kwa usahihi.

**Mwisho,** Nitumie nafasi hii kuwashukuru wote wanaotekeleza afua mbalimbali za kudhibiti UVIDA nchini ikiwa ni pamoja na wizara husika (Afya; Mifugo na Uvuvi; Kilimo; Muungano na Mazingira; na TAMISEMI); hospitali zetu zote zinazoshiriki; vyuo vikuu na taasisi za utafiti;

Vilevile, Wadau wetu wa Maendeleo (WHO, WOAH, FAO, Fleming Fund kupitia ASM, USAID kupitia Breakthrough action na ASLM; na wadau wengine wengi ambao kwa sababu ya muda sitawataja wote ila tunatambua mchango wao kwa dhati kabisa).

**Naamini kwa kutumia dhana shirikishi ya afya moja kwa pamoja tutaelimisha, tutahamasisha na kuchukua hatua stahiki sasa katika kudhibiti na kutokomeza UVIDA.**

Asanteni kwa kunisikiliza!

Limetolewa na



Jenista Mhagama (Mb)

**WAZIRI WA AFYA**

**19/11/2024**